

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S.L.P 02,
USHIROMBO,
BUKOMBE.

MKOA WA GEITA:

Simu: 028 2520709

Barua Pepe: ded@bukombedc.go.tz

Tovuti: www.bukombedc.go.tz



TANGAZO KWA UMMA.

BUKOMBE YAFANIKIWA KUKUSANYA ASILIMIA 85.46 YA MAPATO YAKE YA NDANI.

Halmashauri ya wilaya ya Bukombe imefanikiwa kukusanya asilimia 85.46 ya mapato ya ndani kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 uliomalizika Juni 30 2017.

Katika mwaka huu Halmashauri ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 2,085,657,000.00 Kutoka katika vyanzo vyake vya mapato (own source) ambapo mpaka kufikia mwisho wa mwaka makusanyo halisi ni shilingi 1,782,351,338.48 sawa na asilimia 85.46 ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka mzima

Akizungumza katika Mkutano wa Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Safari Nicas Mayala ametoa pongezi kwa Wakuu wa Idara kwa kuongeza bidii katika kukusanya mapato huku akitoa cheti cha pongezi kwa Mkuu wa Idara ya Misituta Ndugu Stewart Mtondwa kwa kupita lengo la Makusanyo katika idara yake kutoka Milioni 100 hadi kufikia Milioni 300.

Aidha, Mwenyekiti wa Halmashauri amewapongeza pia waheshimiwa madiwani kwa kuwa na ushirikiano mzuri na watendaji hivyo kupelekea matokeo chanya katika kukusanya mapato. "Waheshimiwa tuendeleo kusimamia vyanzo vya mapato ili tuweze kufanya maendeleo kwa wananchi wetu, tuhamasishe wananchi kulipa kodi kwa maendeleo ya Halmashauri yetu" amesema Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Dionis Myinga ameahidi kuendelea kusimamia kwa juhudi na maarifa ukusanyaji wa mapato ambapo kila Mkuu wa idara ambayo inahusika na ukusanyaji wa mapato atasaini Mkataba wa malengo ya ukusanyaji katika idara yake na asiyefikia kiwango tarajiwa hatua za kinidhamu zitachukuliwa. Alisema "Lengo ni kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato ili kuweza kuboresha huduma na kuleta maendeleo kwa wananchi". Pia amesisitiza atasimamia asilimia 10% ya vijana na wakina Mama kutolewa kwa wakati.

Mkutano wa Baraza pia umepokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji na miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kupitisha mpango kazi wa Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Imetolewa Na;
Tusa D Mwambenja
Afisa Habari na Uhusiano.
BUKOMBE.
22/08/2017